

TANGAZO LA SERIKALI Na. 61 la tarehe 26/1/2024

**SHERIA YA MAHAKAMA ZA UTATUZI WA MIGOGORO YA  
ARDHI,  
(SURA YA 216)**

**KANUNI**

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 28C)*

KANUNI ZA MAREKEBISHO YA KANUNI ZA UTEUZI, MALIPO NA NIDHAMU KWA  
MADALALI WA BARAZA NA WASAMBAZA NYARAKA ZA MWAKA 2024

Jina  
T.S Na.  
172 la 2023

**1.** Kanuni hizi zitajulikana kama Kanuni za Marekebisho ya Kanuni za Uteuzi, Malipo na Nidhamu kwa Madalali wa Baraza na Wasambaza Nyaraka za Mwaka 2024 na zitasomwa pamoja na Kanuni za Uteuzi, Malipo na Nidhamu kwa Madalali wa Baraza na Wasambaza Nyaraka za Mwaka 2024 ambazo hapa zitarejewa kama “Kanuni Kuu”.

Marekebisho  
ya kanuni ya 2

**2.** Kanuni kuu zinarekebishwa katika kanuni ya 2 kwa kuongeza tafsiri ifuatayo katika mtiririko wa kialfabeti:

““kukosa uwezo” maana yake ni udhaifu wa mwili au akili uliothibitishwa na daktari anayetambulika na Bodi ya Madaktari;”.

Marekebisho  
ya kanuni ya 3

**3.** Kanuni kuu zinarekebishwa katika kanuni ya 3-  
(a) katika kanuni ndogo ya (4) kwa kufuta aya (d) na kuiandika upya kama ifuatavyo:

“(d) atapoteza sifa au atakosa uwezo wa kuwa mjumbe wa Kamati.”;

(b) kwa kuongeza kanuni ndogo ya (13) kama ifuatavyo:

“(13) Akidi katika kila kikao cha Kamati itakuwa angalau wajumbe watano.”.

Marekebisho  
ya kanuni ya 6

**4. Kanuni kuu zinarekebishwa katika kanuni ya 6 kwa kufuta na kuandika upya kanuni ndogo ya (5) kama ifuatavyo:**

“(5) Msajili atatangaza kwenye tovuti ya Wizara na kwenye magazeti yenye mzunguko mkubwa idadi ya madalali wa mabaraza na wasambaza nyaraka walioteuliwa na Kamati kwa ajili ya mikoa husika ndani ya siku thelathini baada ya uteuzi.”

Marekebisho  
ya kanuni ya  
27

**5. Kanuni kuu zinarekebishwa katika kanuni ya 27-**  
(a) kwa kufuta maneno “mara tu” yaliyopo katika kanuni ndogo ya (1) na badala yake kuweka maneno “ndani ya kipindi cha siku tatu za kazi”;  
(b) kwa kufuta neno “kabla” lililopo katika kanuni ndogo ya (2) na badala yake kuweka neno “ndani”;  
(c) kwa kufuta maneno “iliyolipwa itarudishwa” yaliyopo katika kanuni ndogo ya (4)(c) na badala yake kuweka maneno “pamoja na kiasi kingine chochote kilicholipwa kitarudishwa”.

Dodoma,  
29 Disemba, 2023

JERRY WILLIAM SILAA,  
Waziri wa Ardhi, Nyumba na  
Maendeleo ya Makazi